

# WATOTO WA SHULE YA CHEKECHEA HUPENDA KUJIFUNZA

## Shule ya chekechea ni nini?

Shule ya chekechea ni programu ya elimu kwa watoto kabla hawajaanza shule.

Programu za shule ya chekechea hufundishwa na walimu wenye sifa za shahada. Katika shule ya chekechea, mtoto wako ataendeleza ujuzi muhimu ili kumsaidia kujiandaa kuhudhuria shule.

## Kwa nini mpango wa shule ya chekechea ni muhimu kwa mtoto wangu?

Watoto wanaokwenda shule ya awali wanakuza ujuzi ambao ndio msingi wa masomo yote ya baadaye, kama vile kusoma, kujifunza kuhesabu na kutambua idadi na jinsi ya kutatua matatizo. Mtoto wako atajifunza kuititia kucheza, ambako utafiti unaonyesha ni njia bora ya kuwafundisha watoto wadogo. Katika shule ya awali mtoto wako atafanya marafiki wapya na kujenga ujasiri na uhuru.

## Nani hutoa programu za shule ya chekechea?

Programu za shule za chekechea zinapatikana katika vituo vya utunzaji wa siku nydingi na pia katika huduma za shule za chekechea zinazosimama pekee

## Mimi ninawezaje kuchagua shule bora ya chekechea kwa mtoto wangu?

Ni vizuri kuangalia ikiwa huduma inayotoa shule ya chekechea inayofadhiliwa na serikali - angalia kwenye cheti cha 'Shule ya chekechea' iliyoonyeshwa kwenye huduma hiyo.

Serikali hutathmini ubora wa huduma zote za shule ya chekechea na za siku ndefu chini ya mfumo unaoitwa Mfumo wa Ubora wa Kitaifa na huipa kila huduma kiwango bora. Huduma zote lazima zionyeshe ukadiriaji wao. Unaweza kuuliza huduma kukuonyesha, au kukuambia ni makadirio gani waliyopokea.

Njia bora ya kuhakikisha huduma ni sahihi kwa familia yako ni kutembelea huduma ya utunzaji wa siku ndefu au shule ya awali, kuweza kuangalia karibu na kuzungumza na walimu ili kuelewa ni mpango wa shule ya awali unaweza kumpa mtoto wako.

## Vipi kama bado mtoto wangu hawesi kuzungumza Kiingereza?

Walimu wa shule za chekechea ni pamoja na watoto wote katika mpango huo, hivyo watoto ambao hawazungumzi Kiingereza watakuwa na fursa sawa za kucheza na kujifunza kama wengine.

Baadhi ya shule za chekechea zinaweza pia kuwa na waelimishaji wa lugha mbili ambao wanaweza kutoa msaada wa ziada kwa watoto wanaozungumza kidogo au wasiojua Kiingereza.

## Shule ya chekechea inagharimu kiasi gani?

Serikali inatoa fedha kwa ajili ya watoto wote kuhudhuria masaa 15 ya shule ya chekechea kwa wiki moja kabla ya shule. Huduma nydingi hutoza ada pamoja na ufadhili wa serikali.

Baadhi ya familia wanaweza kupata ruzuku ya kusaidia kwa gharama ya ada za ziada, kwa mfano familia zilizo na kadi za huduma za afya au viza za kibinadamu. Ongea na huduma ya shule ya chekechea kwa maelezo zaidi.

### Ninawezaje kuandikisha mtoto wangu katika shule ya chekechea?

Ikiwa unajua ni huduma gani ya shule ya chekechea ungependa mtoto wako aende kwako unaweza kuwasiliana nao ili kujandidikisha. Halmashauri nyingi nchini zina Miradi ya Uandikishaji wa Shule za Chekechea za Kati ili uweze kuwasiliana na halmashauri yako ya mtaa ili kujandidikisha katika mpango wa shule ya awali katika eneo lako au muulize muuguzi wako wa afya ya mama na mtoto.

Shule nyingi za chekechea huandikisha watoto katikati ya mwaka kwa mwaka uliofufata. Shule nyingi za chekechea zina orodha za kusubiri, kwa hivyo ni wazo nzuri kuandikisha mtoto wako haraka iwezekanavyo ili kupata nafasi nzuri ya kupata nafasi katika mojawapo wa shule za chekechea unayopendelea.

### TAFUTA KUJUA ZAIDI

#### Tovuti

Pata ushauri wa kutafuta shule ya chekechea kwa familia yako:

[www.education.vic.gov.au/parents/childcare-kindergarten/Pages/default.aspx](http://www.education.vic.gov.au/parents/childcare-kindergarten/Pages/default.aspx)

Tafuta shule ya chekechea katika eneo lako:

[www.education.vic.gov.au/findaservice/Home.aspx](http://www.education.vic.gov.au/findaservice/Home.aspx)

#### Simu

Kaskazini mashariki mwa Victoria	1300 333 231
Kaskazini Magharibi mwa Victoria	1300 338 691
Kusini mashariki mwa Victoria	1300 338 738
Kusini Magharibi mwa Victoria	1300 333 232

Ili kupata msaada katika lugha yako:

- Pigia simu Huduma ya Taifa ya Utafsiri pamoja na Ukalimani kwenye namabri 131 450
- Waulize wapige simu namba ya mkoa wako (tazama hapo juu)
- Watabaki kwenye simu na kutafsiri.